




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU



KUMB.NA.MDC/DED/S2/SUBJ/VOL.VIII/2

24 Agosti, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kupitia kibali cha ajira mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/448/01 "A"/62 cha tarehe 22 Julai, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora anawatangazia Nafasi za Kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza Nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

1.1 MTENDAJI WA KIJIKI III (VILLAGE EXECUTIVE III) – NAFASI 2

Nafasi hizi ni kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) AU Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya jamii (Sociology), Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Serikali katika Kijiji
- Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua matatizo/malalamiko na migogoro ya Wananchi katika Kijiji
- Kusimamia Utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji; na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

1.1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS B kwa mwezi

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, S.L.P 74 Mbulu – Manyara,
Simu +255027 2533015 au +255027 2533016 Nukushi +255027 2975124, Barua pepe
md@mbuludc.go.tz. Tovuti www.mbuludc.go.tz


NB: MASHARTI YA JUMLA.

- i. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V)
- iii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu, cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha NIDA vilivyothibitishwa na Wakili au Hakimu wa Mahakama na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport Size) na iandikwe jina nyuma.
- iv. **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- v. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- viii. **Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 6 Septemba, 2021 saa 9.30 Alasiri.**
- ix. Maombi yaandikwe na kusainiwa na mwombaji mwenyewe na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo: -

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU,
S.L.P. 74,
MBULU.**

Tangazo hili pia linapatikana kupitia tovuti ya Halmashauri www.mbuludc.go.tz na ajira.go.tz

Imetolewa na;


Abubakar A. Kuuli
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MBULU.**



Nakala: Katibu,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
Majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na
Eneo la "Asha Rose Migiro Square".
**S.L.P. 2320,
DODOMA.**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, S.L.P 74 Mbulu – Manyara,
Simu +255027 2533015 au +255027 2533016 Nukushi +255027 2975124, Barua pepe
md@mbuludc.go.tz. Tovuti www.mbuludc.go.tz